**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

# MWONGOZO WA UNUNUZI WA KOROSHO GHAFI KWENYE SOKO LA AWALI MSIMU WA 2023/2024 – TOLEO LA NNE


***Imetayarishwa na:-***

Bodi ya Korosho Tanzania,
S. L. P 533,
**MTWARA.**

**Barua pepe:** info@cashew.go.tz
**Nukushi:** (023) 2333536
**Simu ya Bure:** 0800112159


**01 Septemba, 2023**

**MWONGOZO WA UNUNUZI WA KOROSHO GHAFI KWENYE SOKO LA AWALI KWA MSIMU WA 2023/2024 - TOLEO LA NNE**

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali imeweka lengo la kubangua asilimia 60 ya korosho ghafi tani 700,000 zitakazozalishwa nchini ifikapo 2025/2026 na kubangua asilimia 100 ifikapo 2030 ili kufikia agenda 10/30. Ubanguaji wa korosho hapa nchini utasaidia nchi kunufaika zaidi na zao la korosho kwa kuuza korosho iliyoongezwa thamani. Aidha, ongezeko la ubanguaji litasaidia kupanua wigo wa soko la korosho zinazozalishwa hapa nchini pamoja na kuchagiza uzalishaji wa bidhaa zingine zitokanazo na korosho. Pia, ubanguaji wa korosho una mchango mkubwa katika kuongeza ajira hususani kwa wanawake na vijana kwa ujumla.

Ili kufikia lengo hilo, mikakati mbalimbali imewekwa ili kuhamasisha ubanguaji wa korosho hapa nchini. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuanzishwa kwa Soko la Awali ili kuwawezesha wabanguaji wa ndani kununua korosho ghafi bila kushindana na wasafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi *(Exporters)* kwenye minada. Hatua hii ya Serikali inalenga kuwawezesha wabanguaji wa ndani ya nchi kuweza kupata malighafi (Korosho ghafi) za kutosheleza mahitaji ya viwanda vyao. Kwa mujibu wa Mwongozo huu wabanguaji wa ndani ndio watakaoruhusiwa kununua korosho ghafi katika Soko la Awali kwa kiasi cha kutosheleza mahitaji ya mwaka ya viwanda vyao vilivyopo hapa nchini.

## 2.0 MADHUMUNI YA MWONGOZO

Madhumuni ya Mwongozo huu ni kuweka utaratibu utakaowawezesha wabanguaji wa ndani kununua korosho ghafi kwa ajili ya kubangua katika viwanda vyao vya ndani. Pia, masharti ya Mwongozo huu yamelenga kuhakikisha korosho ghafi zote zinazonunuliwa katika mfumo wa Soko la Awali zinabanguliwa hapa chini.

## 3.0 UTARATIBU WA UNUNUZI WA KOROSHO GHAFI KATIKA SOKO LA AWALI

Utaratibu wa ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali nchini unahusisha upatikanaji wa vibali vya ununuzi, mfumo wa uuzaji, udhibiti wa ubora wa korosho, utaratibu wa malipo, usafirishaji na utoaji wa taarifa.

### 3.1 Upatikanaji wa Leseni na Vibali

i. Mbanguaji ataomba leseni ya kununua korosho kwa ajili ya kubangua ***(Buying License for Local Processing)*** ndani ya nchi kupitia mfumo wa kieletroniki ulioko chini ya Wizara ya Kilimo ***(Online Agricultural Trade Management Information System under the Ministry of Agriculture kupitia tovuti www.atmis.kilimo.go.tz)*** akiainisha mahitaji ya korosho ghafi na uwezo wa kiwanda atakachotumia kubangua korosho hizo.

ii. Bodi ya Korosho itafanya tathmini ya maombi ya mbanguaji husika ili

kujiridhisha na uwezo wa kiwanda hicho.

iii. Bodi ya Korosho itasaini Mkataba wa kununua na kubangua korosho ghafi kutoka Soko la Awali na Mbanguaji husika kabla ya kumpatia leseni ya ununuzi wa korosho.

iv. Bodi ya Korosho itaitaarifu Sekretarieti ya Mkoa na Halmashauri ambayo Mbanguaji anataka kununua korosho kwa ajili ya taratibu za utambulisho wa mbanguaji, usimamizi kwenye soko na utoaji wa taarifa za mwenendo wa mbanguaji husika katika ununuzi wa korosho ghafi.

v. Endapo Halmashauri itawasilisha taarifa kwa maandishi, Bodi ya Korosho ikithibitisha Mbanguaji amekiuka taratibu za ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali, Bodi itasitisha leseni ya ununuzi mara moja kwa Mbanguaji husika.

### 3.2 Utaratibu wa Ununuzi wa Korosho Ghafi katika Soko la Awali

i. Ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali (*Primary Market*) utaanza mwezi Septemba, 2023. Ununuzi huu utaenda sambamba hata pale ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Upili (*Secondary Market)* kupitia minada itakayoendeshwa na Vyama Vikuu vya Ushirika utakapoanza hadi hapo viwanda vya ndani vitakapopata malighafi kulingana na mahitaji yao.

ii. Kituo cha kununulia korosho ghafi katika Soko la Awali ni Chama cha Msingi (AMCOS) ikiwa ni pamoja na matawi yake.

iii. Wakulima watakuwa na hiari ya kuuza korosho ghafi katika Soko la Awali au Soko la Upili.

iv. Bei ya korosho ghafi katika Soko la Awali ni ile itakayokubalika baada ya mapatano ya bei *(Negotiation)* kati ya Mkulima na Mbanguaji husika.

v. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho ghafi kwa mkulima moja kwa moja na kisha kulipia ushuru wa Halmashauri (*Crop Cess*), ushuru wa Chama Kikuu cha Ushirika *(Union)*, ushuru wa Chama cha Msingi (AMCOS), mchango wa uendelezaji wa Tasnia ya Korosho nchini kwa Chama Kikuu husika, Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), TARI Naliendele, na gharama ya magunia kama hatakuwa na ya kwake.

vi. Mbanguaji atatakiwa kubangua korosho ghafi zote hapa nchini. Kwa sababu yoyote ile korosho ghafi zilizonunuliwa katika Soko la Awali haziruhusiwi kusafirishwa nje ya nchi zikiwa ghafi.

### 3.3 Uhakiki na Udhibiti wa Ubora wa Korosho Ghafi katika Soko la Awali

i. Uhakiki wa ubora wa korosho ghafi katika Soko la Awali utazingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Ubora wa Korosho uliotolewa na Bodi ya Korosho katika msimu wa mwaka 2023/2024.

### 3.4 Utaratibu wa Malipo

i. Mbanguaji atatakiwa kulipia korosho ghafi alizozinunua moja kwa moja kwa mkulima husika. Malipo kwa mkulima hayatahusisha tozo/gharama zingine zilizoainishwa katika **Kipengele Namba 3.2 (v)**. Tozo zingine zitalipwa katika akaunti za wadau husika kwa utaratibu ulioainishwa katika Mkataba wa kununua korosho ghafi kwenye Soko la Awali.

### 3.5 Usafirishaji

i. Mbanguaji hataruhusiwa kuondosha korosho ghafi hadi wakulima na taasisi husika watapokiri kupata fedha za malipo kwa korosho husika.

ii. Mbanguaji atatakiwa kuomba kibali cha kusafirisha korosho ghafi alizokamilisha malipo yake kwa wakulima na tozo kwa taasisi husika kwa kuandika barua kwenda Bodi ya Korosho Tanzania. Barua hiyo sharti iambatishwe na stakabadhi za malipo ya kwa wakulima na tozo zilizoainishwa kwenye **Kipengele Namba 3.2 (v)**.

iii. Bodi ya Korosho itatoa kibali cha kusafirisha korosho husika kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Hati za Kusafirisha Korosho Nchini.

iv. Mbanguaji atatakiwa kuzingatia taratibu nyingine zote za usafirishaji wa korosho kama zilivyoainishwa katika Mwongozo wa Usimamizi wa Masoko uliotolewa na Bodi ya Korosho kwa msimu wa mwaka 2023/2024.

### 3.6 Utoaji wa Taarifa

i. Mbanguaji atawajibika kutoa taarifa ya ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali kwa Sekretarieti ya Mkoa, Halmashauri husika na Bodi ya Korosho Tanzania kila wiki wakati wote wa msimu.

## 4.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Ili kuhakikisha kuwa changamoto za uhaba wa korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani zinapatiwa ufumbuzi, majukumu ya kiutendaji na kitaasisi yamegawanywa katika makundi mbalimbali ya wadau kama ilivyoelezwa hapo chini.

### 4.1 Wizara ya Kilimo

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya upatikanaji wa korosho ghafi kwa viwanda vya ndani.

ii. Kuunganisha wadau wa Tasnia ya Korosho nchini katika kufikia malengo ya kuongeza thamani na masoko ya korosho inayozalishwa nchini.

### 4.2 Wizara ya Viwanda na Biashara

i. Kutoa na kusimamia miongozo ya kisera juu ya uanzishwaji na uendelezaji wa viwanda vya kubangua korosho nchini.

ii. Kuunganisha jitihada za wabanguaji katika kutafuta masoko ya korosho iliyobanguliwa pamoja na bidhaa zake.

### 4.3 Bodi ya Korosho Tanzania

i. Kupokea maombi ya mahitaji ya korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani kwa kushirikiana na Umoja wa Wabanguaji Wakubwa na Wadogo wa Korosho nchini.

ii. Kuandaa Mkataba ukiainisha mahitaji yaliyowasilishwa na Mbanguaji

iii. Kutoa leseni ya ubanguaji wa korosho kwa wamiliki wa viwanda vya kubangua korosho nchini.

iv. Kutoa leseni ya ununuzi wa korosho ghafi kupitia mfumo wa Soko la Awali.

v. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya zoezi la ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali.

vi. Kusuluhisha migogoro ya ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali.

vii. Kuchukua hatua za kisheria kwa wabanguaji watakaokiuka Mwongozo huu.

### 4.4 Sekretarieti za Mikoa

i. Kuratibu mahitaji ya korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani waliopo katika Mkoa husika.

ii. Kusimamia na kufuatilia zoezi la ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali.

iii. Kutafuta ufumbuzi wa malalamiko/kero za wakulima na wabanguaji katika utekelezaji wa Soko la Awali.

iv. Kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

### 4.5 Ofisi za Wakuu wa Wilaya

i. Kusimamia ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali ndani ya Wilaya husika.

ii. Kuhakikisha kuwa kila Mkulima aliyeuza korosho katika Soko la Awali anapata malipo anayostahili na kwa wakati.

iii. Kuhakikisha kila Mbanguaji aliyenunua korosho kutoka kwenye Soko la Awali anabangua korosho hizo hapa nchini.

iv. Kutafuta ufumbuzi wa malalamiko/kero za wakulima na wengine wanaohusika katika utekelezaji wa Soko la Awali.

v. Kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote atakayebainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali.

**4.6 Halmashauri za Wilaya**

i. Kukusanya mahitaji ya korosho ghafi kwa wabanguaji waliopo kwenye Halmashauri husika.

ii. Kuwatambulisha wabanguaji walioidhinishwa na Bodi ya Korosho kwa AMCOS/Union kwa ajili ya ununuzi wa korosho katika soko la awali.

iii. Kuwezesha Maafisa Ugani wa vijiji/kata kusimamia utekelezaji wa Soko la Awali.

iv. Kufuatilia zoezi la ununuzi wa korosho ghafi kwenye Soko la Awali.

**4.7 Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania**

i. Kusimamia AMCOS na Union ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mwongozo huu.

ii. Kuchukua hatua za kisheria kwa Chama kitakachobainika kukiuka taratibu za utekelezaji wa Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

**4.8 Chama Kikuu cha Ushirika (*Union*)**

i. Kuainisha AMCOS zinazotekeleza Soko la Awali katika msimu husika.

ii. Kusambaza magunia na kamba kwenye AMCOS zinazotekeleza Soko la Awali.

iii. Kufuatilia mwenendo wa ununuzi wa korosho ghafi katika Soko la Awali ndani ya eneo husika.

iv. Kunapokuwa na ushindani wa bei katika Soko la Upili kushirikiana na AMCOS katika kuhakikisha kuwa wabanguaji wa ndani wanapata korosho ghafi za kutosha kwa ajili ya ubanguaji ndani ya nchi.

**4.9 Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS)**

i. Kuratibu mapatano ya bei kati ya Mkulima na Mbanguaji anaehitaji kununua korosho ghafi katika Soko la Awali.

ii. Kusimamia malipo ya korosho ghafi kwa wakulima waliouza korosho ghafi kupitia Soko la Awali.

iii. Kuhakikisha kuwa korosho zitakazouzwa na wakulima katika Soko la Awali zinakidhi viwango vya ubora kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi na udhibiti Ubora wa Korosho wa mwaka 2023/2024.

iv. Kukusanya tozo mbalimbali zinazostahili ikiwa ni pamoja na ushuru wa AMCOS, ushuru wa Union, gharama ya magunia na kulipa kwa wahusika kwa wakati unaostahili.

v. Kuhakikisha malipo kwa wakulima waliouza korosho ghafi katika Soko la Awali yanafanyika ndani ya siku mbili tangu siku ya mapatano ya bei.

vi. Kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusiana na malipo ya korosho ghafi zilizonunuliwa kupitia Soko la Awali.

vii. Kutoa taarifa kwa wakati kwa Mkuu wa Wilaya, Bodi ya Korosho Tanzania, Halmashauri na Chama Kikuu cha Ushirika juu ya ukiukwaji wowote wa taratibu za Soko la Awali kwa mujibu wa Mwongozo huu.

### 4.10 Mbanguaji wa Ndani

i. Kuainisha mahitaji ya korosho ghafi na kuwasilisha Bodi ya Korosho na Halmashauri anayotaka kununua korosho.

ii. Kuwasilisha maombi ya leseni ya kununua korosho ghafi kutoka kwenye Soko la Awali kwa Bodi ya Korosho akiainisha Halmashauri atakazonunua korosho.

iii. Kushirikiana na Umoja wa Wabanguaji Wakubwa au Wadogo katika ununuzi wa korosho ghafi na upatikanaji wa masoko ya korosho zilizobanguliwa ndani na nje ya nchi.

iv. Kuwasilisha taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Mwongozo huu kwa Bodi ya Korosho Tanzania.

v. Kubangua korosho zote atakazonunua kutoka kwenye Soko la Awali.

vi. Kuzingatia gharama za uzalishaji wa korosho ghafi ikiwa ni pamoja na faida kwa mkulima/wakulima husika wakati wa mapatano ya bei ya kununulia korosho kutoka kwenye Soko la Awali.

vii. Kutunza kumbukumbu za malipo aliyoyafanya kwa korosho alizonunua kutoka kwenye AMCOS husika.

### 4.11 Umoja wa Wabanguaji wa Korosho nchini TACP na UWWKT

i. Kusimamia na kuhakikisha kwamba korosho zinazonunuliwa kupitia Soko la Awali zinabanguliwa hapa nchini.

ii. Kutoa taarifa ya mwenendo wa ubanguaji wa korosho nchini kila mwezi kwa Bodi ya Korosho.

iii. Kutoa taarifa Bodi ya Korosho/Halmashauri za Wilaya juu ya changamoto zozote zinazojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu na mapendekezo ya namna ya kuzitatua changamoto hizo.

iv. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu miongoni mwa wanachama wa TACP au UWWKT.

**4.12 Mkulima wa Korosho**

i. Ana hiari ya kuuza korosho ghafi kwenye Soko la Awali.

ii. Kuvuna korosho ghafi na kupanga katika madaraja kabla ya kupeleka katika AMCOS kwa ajili ya uuzaji kwa Mbanguaji.

iii. Kushiriki mapatano ya bei ya kuuzia korosho ghafi kwenye Soko la Awali.

iv. Kuepuka kuchanganya korosho na vitu visivyo korosho ikiwa ni pamoja na korosho zilizoharibika.

v. Kuzingatia gharama za uzalishaji wa korosho wakati wa mapatano ya bei.

vi. Kutoa taarifa kwa mamlaka husika pale inapotokea ukiukwaji wowote wa taratibu za Mwongozo huu.

**4.13 Taasisi za Fedha (Mabenki)**

i. Kutoa huduma za fedha kwa wakulima na wabanguaji ili waweze kufikia malengo yao.

ii. Kuhamasisha wakulima na wabanguaji kutumia huduma za kibenki.

iii. Kuwatembelea na kuwafungulia akaunti wakulima kwa ajili ya kupokelea malipo ya korosho.

iv. Kutoa uthibitisho wa mbanguaji kuweza kufanya malipo ya korosho atakazonunua katika soko la awali.

**5.0 MAKOSA NA ADHABU**

i. **Kununua korosho kwenye Soko la Awali bila kibali.** Korosho husika zitataifishwa kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009 na Kanuni za Mwaka 2010.

ii. **Kuchelewa kufanya malipo kwa mkulima.** Mkulima kupitia AMCOS husika anaruhusiwa kuuza kwa mbanguaji mwingine au Soko la Upili (Mnada). Sambamba na hili; mbanguaji husika atazuiwa kununua korosho ghafi kutoka kwenye Soko la Awali kwa kipindi cha msimu mzima.

iii. **Kusafirisha korosho ghafi zilizonunuliwa kwenye Soko la Awali kwenda masoko ya nje ya nchi.** Korosho husika zitataifishwa na Bodi ya Korosho ikiwa ni pamoja na kusitisha kibali cha ununuzi wa korosho ghafi kutoka Soko la Awali kilichotolewa kwa mbanguaji husika.

## 6.0 HITIMISHO

### 6.1 Wajibu wa Pamoja

i. Kuhakikisha kuwa madhumuni na utekelezaji wa Mwongozo huu yanazingatia Sera na Sheria za Nchi.

ii. Kutoa taarifa mapema kuhusu suala lolote litakaloathiri utekelezaji wa Soko la Awali.

iii. Kuhakikisha Soko la Awali linakuwa na manufaa kwa wadau wote kuanzia wakulima hadi wabanguaji.

iv. Kuhakikisha kila mdau anatimiza wajibu wake kwa mujibu wa Mwongozo huu.

v. Kushirikiana katika eneo lolote linalofanikisha upatikanaji wa korosho ghafi kwa ajili ya viwanda vya ndani.

### 6.2 Muda wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Mwongozo huu ni kuanzia tarehe 01 Septemba 2023 hadi 30 Agosti 2024.

### 6.3 Ilani

Serikali haitawajibika kwa namna yoyote ile kwa mdau/mhusika ambaye hatazingatia utaratibu uliowekwa katika Mwongozo huu.

### 6.4 Mwisho

Mwongozo huu unasomwa sambamba na Sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya Mwaka 2009, Kanuni zake za Mwaka 2010 pamoja na Miongozo mingine itakayotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania.

Mwongozo huu umetolewa leo tarehe 01 SEPTEMBA, 2023

.....................................

Francis Alfred

**MKURUGENZI MKUU**